**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**687 VITENDO VYA KUJIFUNZA HAIBA NA MICHEZO**

**Muda: Saa 3.** **Alhamis 08 Mei 2014 mchana**

**Maelekezo.**

1. Karatasi hii ina sehemu **A** na **B** zenye jumla ya maswali **kumi na sita (16)**.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu **A** na maswali **manne (4)** kutoka katika sehemu **B.**
3. Sehemu A ina alama **arobaini (40)** na sehemu B ina alama **sitini (60)**
4. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Eleza sababu nne zinazoweza kumfanya mtoto wa Elimu ya Awali kushindwa kushiriki kikamilifu katika michezo ya darasani.

2. Fafanua kwa kifupi aina nne za michezo ya kitamaduni inayoweza kutumika kufundisha tabia njema.

3. Bainisha kwa kifupi umuhimu wa kufanya tathmini endelevu kwa watoto wa Elimu ya Awali katika somo hili. Toa hoja nne.

4. Eleza hatua nne anazopaswa kufuata mwalimu katika kuchagua eneo la kuchezea linalofaa kwa ajili ya michezo ya nje.

5. Onyesha namna nne ambavyo michezo inaweza kutumika kama nyenzo muhimu ya kukuza lugha kwa watoto wadogo.

6. Taja na ufafanue kwa kifupi vipengele vinne vinavyopatikana katika Azimio la Kazi la Vitendo Vya Kujifunza Haiba na Michezo.

7. Eleza kwa kifupi maana ya Utu Uzima kama dhana inavyofundishwa kwa watoto wa Elimu ya Awali. Toa hoja nne.

8. Changanua vyanzo vinne vya kanuni za nidhamu ambazo mwalimu wa Elimu ya Awali anaweza kuzitumia kuongoza michezo.

9. Fafanua kwa kifupi aina nne za zana za kufundishia zinazotegemea mazingira asilia ambazo mwalimu anaweza kutumia.

10. Eleza kwa kifupi faida nne za kupanga michezo ya kufundisha ikizingatia **malengo maalum** ya somo.

**SEHEMU B (Alama 60)**

Jibu maswali **manne (4)** kutokasehemu hii

11. Kwa kutoa hoja tano jadili jinsi ushirikishwaji wa wazazi unavyoweza kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya Vitendo Vya Haiba na Michezo.

12. Fafanua mambo matano yanayopaswa kuzingatiwa katika kuandaa mazingira salama kwa ajili ya michezo ya watoto wa Elimu ya Awali.

13. Eleza kwa kina mbinu tano za kidemokrasia ambazo mwalimu anaweza kuzitumia katika kusimamia nidhamu darasani bila kutumia viboko.

14. Ufundishaji shirikishi huimarisha uelewa wa watoto. Tetea kauli hii kwa kutumia hoja tano.

15. Changanua kwa kina vipengele vitano vya Maendeleo ya Mtoto ambavyo huathiriwa moja kwa moja na ushiriki wake katika Vitendo Vya Kujifunza Haiba na Michezo.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org